

# DAREM the Lion Defender

written by: Amy Dickman and Alayne Cotterill  
illustrated by: Kayla Harren






For Millie and Rufus  
and children everywhere.

We hope you  
grow up in a world  
that is good for both  
people and lions.

# DAREM the Lion Defender

written by: Amy Dickman and Alayne Cotterill  
illustrated by: Kayla Harren






Darem ni kijana anayetokea kwenye kabila la Wabarabaig. Anaishi katika kijiji karibu na eneo la uhifadhi. Ana kaka zake wawili wanaitwa Mandela na Daudi na mdogo wake wa kiume mmoja anaitwa Shabani. Shabani ni kijana mdogo sana na mara nyingi huwa anaumwa. Darem hupata hofu kwenye hili na kufanya afikiri cha kufanya ili kusaidia familia yake.

Darem is a boy from the Barabaig tribe. He lives in a village close to a protected area. He has two older brothers called Mandela and Daudi and a younger brother called Shabani. Shabani is quite small and often gets sick. Darem worries about this and wishes there was something he could do to help his family.

Darem hutumia muda mwingi kuangalia ng'ombe wa familia yao.  
Watu humwambia aangalie simba, kwa sababu ni wabaya na  
hatari, lakini hajawahi kuona hata mara moja.

Darem spends most of his time watching over his family's cattle.  
People tell him to look out for lions as they are bad and dangerous,  
but he has never seen one.



Siku moja aliona nyayo za simba.  
Alifuatilia kidogo walimopita, na mbele  
akaona simba jike. Darem aliogopa,  
lakini simba hakumuona kwa hiyo  
akabaki amesimama wima.

One day he spots lion tracks. He follows  
them for a little way, and sees a lioness.  
Darem feels scared, but the lioness has  
not seen him so he just stands very still.






Ghafla watoto watatu wa simba walitoka kichakani, wakifukuzana kila mmoja kama Darem anavyofanyaga na kaka zake. Darem aliendelea kuwaangalia wakicheza, alijisikia raha na hofu ilipungua.

Three lion cubs suddenly run out of the bush, chasing each other like Darem does with his brothers. Darem watches them play, and feels excited and less scared.







Darem huangalia simba kila siku. Muda mwingine hufuatilia nyayo hadi mtoni, na kama akisimama kwa umakini anaweza kuona simba wakicheza. Simba na watoto wake huonekana wakipendana sana kama Darem anavyopenda familia yake.

Darem looks for the lions every day. He often finds their tracks by the river and, if he sits very still, he can watch them play. The mother and cubs seem to love each other just as Darem loves his own family.


Mtoto mmoja wa simba ni mdogo kuliko simba wengine. Humkumbusha Darem kuhusu mdogo wake aitwaye Shabani.

One cub is smaller than the others. He reminds Darem of his little brother so he calls it Shabani.



Lakini simba mwenye watoto na watoto wake wameendelea kuwa wembamba. Shabani huonekana mwenye huzuni na njaa. Darem huonekana mwenye huzuni na kaka zake huwa na njaa pia. Hustaajabu namna gani anaweza kuwasaidia.

But over time the mother and cubs get thinner. Shabani in particular looks sad and hungry. Darem feels sad as he and his brothers are often hungry too. He wonders what he can do to help.



Usiku mmoja, Darem alilala kwenye kibanda chake. Alisikia kelele zikipigwa na akatoka nje pamoja na kaka zake. Kumbe simba alivamia ng'ombe wao kwenye boma. Alivyoona zile nyayo za simba akagundua ni ni yule simba jike na watoto wake ambao huwafuatilia nyayo zao kila siku.

Baba yake na kaka zake wana hasira, kwa ng'ombe wao kuuawa. Darem anajiskia huzuni kwenye familia yake, lakini anajiskia huzuni kwa simba pia, kwa sababu anajua simba huyo alikuwa na njaa na alikuwa anawalisha watoto.

Kaka zake wanasema watatafuta kundi la vijana, na kwenda kuwinda wale simba. Wanafikiri kuwa kama wakiuwa simba mifugo yao itakuwa salama na kijiji kitakuwa na furaha.



One night, Darem is sleeping in his hut. He hears shouting and runs outside with his older brothers. A lion has attacked his family's cattle enclosure. When he sees the lion tracks, he realizes they are those of the mother lion he has tracked every day. His father and brothers are angry as one of their cows has been killed. Darem feels sad for his family, but he also feels sorry for the lion too as he knows she is hungry and is only trying to feed her cubs.

His brothers say they will get a group of warriors together and go out to hunt the lion. They think that if they kill the lion their livestock will be safer and the village will be happy.



Darem anajisikia huzuni sana. Anajua watoto wa simba watakufa kama mama yao atauwawa, na Shabani yule mtoto wa simba ni mdogo sana kukimbia toka kwa wawindaji.

Anajisikia anatakiwa aokoe ile familia ya simba.

Darem feels very worried. He knows the cubs will die if their mother is killed, and Shabani the lion cub is too small to run away from the hunters.

He feels he has to try to save the lion family.



Darem aliwasikia watu kutoka Mradi wa Lion Landscapes, kuwa wanawasaidia watu na wanyama kama simba. Mapema asubuhi sana alitembelea kambi yao iliyopo kijijini.

Anahamanika kuongea na watu ambao hajawahi onana nao. Lakini hawa watu walikuwa ni rafiki kwake pale alipoanza kuongelea uvamizi wa simba na mipango ya uwindaji. Mtu mmoja aitwaye Stephano alienda nyumbani kwao kuwasaidia.

Darem has heard about people from Lion Landscapes who help people and animals like lions. He decides to walk to their camp in the village. He is nervous about talking to strangers. But they are friendly and, when he explains about the lion attack and planned hunt, a kind man called Stephano comes to his house to help.



Mradi wa Lion Landscapes umezuia ng'ombe wa baba yake kuvamiwa tena kwa kuwajengea boma imara la waya. Stephano aliwapa namba yake ya simu na kila mtu akawa na furaha. Darem huenda kulala akijua kuwa familia yake ipo salama na simba pia wapo salama.

Lion Landscapes protects his father's cattle enclosure with wire to stop any more attacks. Stephano gives them his phone number and everyone is happy. Darem goes to bed thinking that his family and the lions are safe.









Asubuhi nyingine tena, Darem alisikia Mandela na Daudi wakiondoka nyumbani kwao. Kwa ukimya akawafuata, akawaona wamechukua mikuki. Na walikuwa na vijana wengine wa kiume, na Darem akagundua kuwa bado wanaenda kuwinda yule simba na watoto wake.

Early the next morning, Darem hears Mandela and Daudi leaving the house. He silently follows them, and sees they carry many spears. They meet with other young men, and Darem realizes they are still going to try to spear the lioness and her cubs.




Alichanganyikiwa sana na wale simba na hakujua nini afanye. Akakumbuka kuwa ana namba ya simu ya Stephano. Akarudi nyumbani kwao, na akatumia simu ya baba yake kumpigia Stephano na kumueleza kuhusu mpango ule wa uwindaji.

He is very frightened for the lions and does not know what to do. Then he remembers he still has Stephano's phone number. He goes back to his house, and uses his father's phone to call Stephano and warn him about the lion hunt.

Darem alienda mtoni akakaa huko lakini familia ya simba haikuja tena. Anataka simba wawe salama lakini pia hapendi kaka zake wawe kwenye matatizo. Alikuwa na hofu sana, ameenda kinyume kabisa na familia yake pamoja na kabila lake!?

Darem goes to the river and waits for the lions, but they do not come. He is very worried. He wants the lions to be safe but does not want his brothers to get into trouble. Has he gone against his family and his tribe?



Jioni wakati jua likizama kaka zake walirudi nyumbani. Darem anajificha kwa sababu kaka zake watakuwa na hasira juu yake kwa kuwasaidia simba. Lakini walitabasamu na kumuita.

At sunset his brothers finally come home. Darem is hiding because he is afraid they will be angry with him for helping the lions. But they are smiling and Mandela calls to him.





Wakamwambia kuwa kundi la vijana wanaitwa Walinzi wa Simba kutoka Mradi wa Lion Landscapes wamekutana na wawindaji, na kuongea nao kuwa waache kuwinda. Walinzi wa Simba walieleza kuwa walikuwa wanawinda simba lakini sasa wamepata kazi ya kulinda simba. Kaka zake Darem wakaanza kujaribu kujiunga na Mradi wa Lion Landscapes kama Walinzi wa Simba.

They tell him that a group of warriors called Lion Defenders from Lion Landscapes met up with the hunters, talked with them and got them to stop the hunt.

The Lion Defenders explained that they used to hunt lions but now have jobs protecting lions. Darem's brothers decided to try joining Lion Landscapes as Lion Defenders.





Kaka zake Darem wakawa walinzi wazuri sana wa simba. Wanafuatilia simba, wanazuia jamii kuuwa simba na wanasaidia wanavijiji kutafuta mifugo iliyopotea. Kila mwezi wanapokea hela, zinazosaidia familia nzima. Wanakuwa watu muhimu kwenye kijiji.

Darem's brothers become excellent Lion Defenders. They track lions, protect the community and help villagers find lost livestock. Every month they earn money, which helps the whole family. They become important people in the village.







Darem anaona kuwa Mradi wa Lion Landscapes unasaidia watu na simba kwa namna nyingi. Wanafanya kazi na wanavijiji kutega kamera porini. Kama kamera zikinasa picha za wanyamapori kijiji chote hupata faida. Simba wakiwa wengi, ndivyo faida nyingi watu hupata. Darem anaongea na maafisa utegaji kamera kwenye kijiji chao. Anawaonesha sehemu ambako amekuwa akiona familia ya simba. Darem anataka simba walete faida za kutosha kijijini.

Darem sees that Lion Landscapes helps people and lions in many different ways. They work with villagers to put out camera-traps in the bush. If the camera-traps photograph wild animals, the whole village gets benefits.

The more lions there are, the more benefits people receive.

Darem talks to the camera-trapping officer in his village. He shows him where he always sees his lion family. Darem wants his lions to bring the village lots of benefits.





Kuna ushindani mkubwa katika vijiji kuwa nani anaweza kuwa na wanyamapori wengi. Kijiji cha Darem kimeshinda kwa sababu ya picha za simba aliowaona!

There is a competition between all the villages to see who has the most wildlife. Darem's village wins because of the photos of his lioness and her cubs!



Huwa kuna sherehe na kijiji hupokea madawa kwa ajili ya watu na ng'ombe, na shule hupokea vitabu.

There is a celebration and the village receives medicines for people and cattle, and books for the school.



Dawa zimesaidia mdogo wake Shabani kuweza kupona. Anavyozidi kukua, Darem anaona mdogo wake anakuwa mnene na mwenye nguvu.

The medicine helps Darem's brother Shabani get better. As he grows up, Darem sees his little brother become big and strong.



Ile familia yake ya simba imeachwa salama na ni muhimu kwa jamii, na Shabani anakua na simba wazuri.

His lion family is kept safe as it is important to the community, and Shabani grows into a beautiful lion.



Darem anajisikia fahari na furaha sana. Amesaidia simba na kijiji chake. Kwa sasa anajua kuwa simba wana manufaa kwa watu, ila simba hao pia wanahitaji msaada wa watu.

Darem anaamua kwamba akikua anataka ajiunge na Mradi wa Lion Landscapes ili awe mlinzi wa simba mwenye ujasiri kama kaka zake. Ana ndoto za kuona siku simba na binadamu wanaishi pamoja kwa furaha, na amejitoa kusaidia.

Darem is very proud and happy. He has helped the lions and his village. He now knows that lions can help people, but they need people to help them too. Darem decides that when he is older he wants to join Lion Landscapes and become a brave Lion Defender like his brothers. He dreams of a time when lions and people can live together happily, and is determined to help make that dream come true.





## UKWELI KUHUSU SIMBA Simba ni wanyama wa ajabu sana – jifunze kuhusu wao... Lion Facts! Lions are amazing animals – learn more about them

- Simba ni paka wa pili kwa ukubwa duniani, baada ya tiger. Simba dume ana uzito kati ya kilo 180-ambao ni sawa na uzito wa vijana 6 wenye miaka 10.

Lions are the second biggest cat in the world, after tigers. Males can weigh around 180kg – that is about the same weight as six 10-year old boys!

- Simba ni paka pekee wanaoishi kwenye makundi, yaitwayo familia. Mara nyingi familia huundwa na majike kati ya 3-18 na simba dume kuanzia 1-9, pamoja na watoto wao.

Lions are the only cats that live in groups, called prides. Prides usually consist of 3-18 females and 1-9 males, as well as their cubs.

- Kama ilivyo kwa paka wengine wakubwa, simba anaweza unguruma lakini hawezi kutoa sauti nyembamba. Muungurumo wao unaweza kwenda hadi kilometa nane na unakaribiana na ule wa radi.

Lions, like other big cats, can roar but they cannot purr. Their roar can be heard up to 8 kilometres away and is nearly as loud as thunder.

- Unaweza kutambua miaka ya simba kwa kutumia rangi ya pua yake! Jinsi miaka inavyoongezeka, rangi za pua zao hubadilika kutoka pinki hadi kuwa nyeusi.

You can tell the age of a lion by the colour of its nose! As lions age, their noses go from pink to black.



- Unaweza kutambua simba mmoja mmoja kwa kuangalia doti za sharubu zake pembeni mwa pua yake.

Hii ni kama alama ya vidole, ambapo simba wawili hawawezi kufanana kwa kungalia doti zao.

You can tell individual lions apart by looking at the 'whisker-spots' on the side of their noses. These are like a fingerprint, with no two lions having the same pattern of spots.

- Kwa kuongelea doti zao, doti za simba wadogo huonekana vizuri! Doti hizi huendelea kupotea jinsi wanavyokua, lakini unaweza kuendelea kuziona ubavuni mwa tumbo na kwenye miguu ya simba wakubwa.

Talking of spots, lion cubs start off very spotty! These spots fade as they grow up, but you can often still see some spots on the bellies and legs of adult lions.

- Simba dume ni paka pekee wenye manyoya marefu shingoni. Inasemekana manyoya haya husaidia simba kwenye mapigano, na kujionesha kwa majike - ambao huonekana kupenda simba wenye manyoya marefu, na meusi.

Male lions are the only cats which have manes of long hair. Manes are thought to protect lions in fights, and to show off to females – who seem to prefer males with long, dark manes.

- Kihistoria, simba walikuwepo duniani kote hata Amerika na Ulaya. Kwa sasa simba wanaishi Afrika, na idadi ndogo wamebaki India. Tanzania ni nchi muhimu sana iliyobaki na simba wa porini.

Historically, lions lived across the world, including America and Europe. The modern lion mainly lives in Africa, with one small population left in India. Tanzania is the most important country left for wild lions.

- Idadi ya Simba wamepungua katika kipindi cha miaka 20 iliyopita. Jinsi ongezeko la watu linavyozidi, ndivyo wanavyokosa makazi yao na chakula. Mashirika kama Lion Landscapes unafanya kazi mhimu kusaidia kuhifhadi simba waliobaki porini.

Lion numbers have halved in the past 20 years. As human populations grow, they are running out of space and food. Organisations like Lion Landscapes play an important role in helping protect remaining wild lions.

## Lion Conservation & Lion Landscapes

Simba wako katika matatizo makubwa, idadi yao imepungua kwa karibu miaka 20 na sasa kuna simba wachache katika Afrika kuliko Faru. Simba na wanyama wengine wanategemea sana ardhi iliyo nje ya ulinzi wakati maranyingi wanashambulia mifugo na matokeo yake kuuwawa.

Lion Landscapes inafanya kazi na jumuiya za nchi ambazo ni Kenya, Zambia na Tanzania kusaidia watu na wanyamapori kuishi pamoja kwa urahisi zaidi.

Ni matumaini yetu kuwa hadithi hii itasaidia vizazi vijavyo kuwa na uwelewa mzuri kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa jamii. Faida yoyote itasaidia utendaji wa kazi zetu za uhifadhi.

Lions are in serious trouble, their numbers have halved in around 20 years and there are now fewer wild lions in Africa than rhinos. Lions and other species rely heavily on land outside protected areas where they sometimes attack livestock and are often killed as a result.

Lion Landscapes works with local communities in Kenya, Zambia and Tanzania to help people and wildlife live alongside one another more easily.

We hope this story will help young people better understand the importance of community conservation. Any profits will be used to support our field conservation work, see [www.lionlandscapes.org](http://www.lionlandscapes.org).



## Illustrator Kayla Harren


Kayla ameonyesha picha za vitabu vingi vya watoto, ikijumuisha Haikya rafiki wa Fisi, pia Lion Landscapes. Kuona mengi kuhusu kazi ya Kayla, tembelea tovuti [www.kaylaharren.com](http://www.kaylaharren.com).

Kayla has illustrated several picture books for children, including Haikya the Hyaena Friend, also by Lion Landscapes. To see more of Kayla's work, visit [www.kaylaharren.com](http://www.kaylaharren.com).

## Become a Lion Landscapes Champion

Kama utapenda kusaidia kazi zetu, soma neno siri hili au tembelea tovuti yetu ili kujua zaidi.

If you would like to support our work, scan this code or visit our website to find out more.



With thanks to the following who helped produce this storybook:



Supported by IUCN Save Our Species,  
co-funded by the European Union

Darem is a young boy from the Barabaig tribe and lives in Africa where he spends most of his time herding his family's cattle. People say he should be scared of dangerous animals like lions, but Darem starts to think differently as he comes to know and love a small family of lions living on village land. However, he struggles when protecting the lions seems to go against his family and his tribe. Can Darem find a way of helping his lions, his family and his whole community?

This heart-warming tale, enchantingly illustrated by Kayla Harren, will give children across the world an insight into the plight of lions and those who live alongside them. It highlights the work of Lion Landscapes, a UK charity doing community-based conservation in incredible wild landscapes.

Thank you for helping both lions and people.



Lion Landscapes is proud to be climate positive and offsets double its carbon emissions using Lion Carbon [www.lioncarbon.org](http://www.lioncarbon.org)

ISBN 978-1-9161916-2-4



9 781916 191624 >